




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA



Simu: +255 (026) 2650019 (G/L)
+255 (026) 2650021 (D/L)
Nukushi: +255 (026) 2650242
Barua pepe: ded@igungadc.go.tz
Tovuti: <http://www.igungadc.go.tz>

Halmashauri ya Wilaya ,
S.L.P 19,
IGUNGA.

Unapojibu tafadhari taja

Kumb. Na. HWIG/C.2/3/28

23 Novemba, 2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga amepokea vibali viwili vya ajira mbadala vyenye Kumb. Na. FA.170/365/01"B"/22 ya tarehe 14 Agosti, 2020 na FA.170/365/01"B"/38 ya tarehe 06 Novemba, 2020 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika nafasi zifuatazo;-

1. Watendaji wa Vijiji Daraja la III nafasi (02)
2. Katibu mahsusi Daraja la III nafasi (02)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Igunga anakaribisha ya maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi 04 wazi za kazi kama ilivyoainishwa katika Tangazo.

1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III NAFASI 02 (VILLAGE EXECUTIVE GRADE III)

1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- i. Mtendaji na mshauri wa Halmashauri ya Kijiji na kamati zake katika mipango ya maendeleo ya Kijamii na Utekelezaji wa Mipango ya maendeleo.
- ii. Afisa Masuuli na mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
- iii. Mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora Katika Kijiji
- iv. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- v. Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji.

